# صِفَاتُ

# الزَّوْجَةِ الصَّالِحَةِ

# SIFA ZA MKE MWEMA


**Imeandaliwa na:**

**Abu Halima Arafat Bin Mahmoud**

**Pongwe – Tanga**

**Tanzania.**

بسم الله الرحمن الرحيم

Kila sifa njema anastahiki Allaah Ta'alaa na swala na salamu zimshukie Mtume, Jamaa zake na Maswahaba walio wema.

Ewe Mama/Dada yangu wa Kiislamu endapo utasimama imara kutekeleza amri za Allaah na kuacha makatazo yake kisha ukatimiza haki za Mume wako ipasavyo wewe ni sehemu kubwa ya starehe kwake hapa duniani kwa ushahidi wa hadithi:

«الدُّنْيَا مَتَاعٌ، وَخَيْرُ مَتَاعِ الدُّنْيَا الْمَرْأَةُ الصَّالِحَةُ»

**"Dunia yote ni starehe na bora ya starehe za dunia (kupata) Mke mwema[1]".**

Kinyume chake ni kwamba ukipata mke muovu umekosa starehe yote ya dunia na hiyo ni hali ya nyumba nyingi za waislamu, wanaume wengi wanaishi kwa mawazo, simanzi na kutawaliwa na huzuni kwa sababu ya kukosa mke mwema, nyumba zao zimegeuka viwanja vya mapambano kwa matusi, kejeli, dharau na wengine hupata kichapo kutoka kwa wake zao!. Ndiyo maana Mtume wetu akasema:

«فَاظْفَرْ بِذَاتِ الدِّينِ، تَرِبَتْ يَدَاكَ»

**"Pupia (kuchagua) mwanamke mwenye dini, itabarikiwa mikono yako[2]".**

Amesema Imam Nnawawi Allaah amrehemu:

(وَفِي هَذَا الْحَدِيثِ الْحَثُّ عَلَى مُصَاحَبَةِ أَهْلِ الدِّينِ فِي كُلِّ شَيْءٍ لِأَنَّ صَاحِبَهُمْ يَسْتَفِيدُ مِنْ أَخلَاقِهِمْ وَبَرَكَتِهِمْ وَحُسْنِ طَرَائِقِهِمْ وَيَأْمَنُ الْمَفْسَدَةَ من جهتهم)

---

1- Muslim (1467).

2- Bukhari (5090) na Muslim (1466).

**"katika hadithi hii kuna himizo la kusuhubiana na watu wenye dini katika kila jambo, kwa sababu mwenye kufanya usuhuba na watu hao atafaidika kwenye tabia zao, Baraka na uzuri wa mwenendo wao na atasalimika na madhara kutoka upande wao[3]".**

Ewe mwanamke wa Kiislamu zingatia hadithi zilizo tangulia pamoja na maelezo yake, na fahamu kwamba huo ni wajibu wako wala si hiyari, na kupata ridhiaa ya mume wako ni sababu ya kukubaliwa amali zako mbele ya Allaah Subhaanah.

Amesema Ibnul Jauziy Allaah amrehemu:

(وَيَنْبَغِيْ لِلْمَرْأَةِ العَاقِلَةِ إِذَا وَجَدَتْ زَوْجاً صَالحِاً يُلَائِمُهَا أَنْ تَجْتَهِدَ فِيْ مَرْضَاتِهِ، وَتَجْتَنِبَ كُلَّ مَا يُؤْذِيْهِ، فَإِنَّهَا مَتَى آذَتْهُ، أَوْ تَعَرَّضَتْ لِمَا يَكْرَهُهُ أَوْجَبَ ذَلِكَ مَلَالَتَهُ، وَبَقِيَ ذَلِكَ فِيْ نَفْسِهِ، فَرُبَّما وَجَدَ فُرْصَتَهُ فَتَرَكَهَا أَوْ آثَرَ غَيْرَهَا، فَإِنَّهُ قَدْ يَجِدُ، وَقَدْ لَا تَجِدُ هِيَ، وَمَعْلُوْمٌ أَنَّ المَلَلَ لِلْمُسْتَحْسِنِ قَدْ يَقَعُ، فَكَيْفَ لِلْمَكْرُوْهِ؟).

**"Inapasa kwa mwanamke mwenye akili akipata mume mwema anaemfaa ajitahidi kumridhisha (kumfurahisha) na kujiepusha na kila lenye kumchukiza, kwa sababu yeye wakati wowote atakapomuudhi au kufanya jambo lenye kumchukiza litapelekea hilo kumhuzunisha/kuchoka na litabaki hilo ndani ya moyo wake, na huenda huyo (mume) akapata fursa yake akamuacha au akamfadhilisha mwingine, kwa sababu huenda huyo (mume) akampata (mke mwingine) na yeye (mke) huenda asipate (mume kama huyo), na ni jambo lenye kujulikana kwamba kuchoshwa huenda kukapatikana hata kwa mwenye kutenda wema basi vipi kwa mwenye kuchukiza?![4]".**

Wabilaahi Ttaufiiq.

---

[3]- Sharhi Muslim (Jz. 10, Uk. 54).

[4]- Angalia kitabu: [Ahkaamu Nnisaa (Uk. 145)].

**Sifa hizo ni:**

1. Kudumu katika kumtii Allaah Ta'alaa kwa kutekeleza haki zake ambazo ni swala, saumu, kujichunga na zinaa, kuvaa hijabu, kuinamisha macho (kuacha kutazama haramu) n.k.
2. Kujichunga wakati mume wake anapokuwa hayupo, asije kuonekana au kusikika na watu ambao si mahaarim zake.

Allaah amesema:

﴿فَٱلصَّٰلِحَٰتُ قَٰنِتَٰتٌ حَٰفِظَٰتٌ لِّلۡغَيۡبِ بِمَا حَفِظَ ٱللَّهُۚ﴾

**[Basi wanawake wema ni wale wenye kutii, wanao jilinda hata katika siri (wakiwa mbali na waume zao) kwa vile Allaah alivyoamrisha wajilinde[5]].**

3. Kumtii mume katika jambo ambalo hakuna ndani yake kumuasi Allaah na kutekeleza haki zake kikamilifu.

Amesema Mtume swala na salamu zimshukie:

«لَا طَاعَةَ لِمَخْلُوقٍ فِي مَعْصِيَةِ الْخَالِقِ»

**"Hakuna kumtii kiumbe yeyote katika kumuasi (Allaah) Muumba[6]"**

4. Kumtumikia mume wake: na jambo la kwanza hapa ni kusimamia malezi ya watoto nyumbani, usafi wa nyumba, kuandaa chaku n.k.

Amesema Ibn Taymiyyah (Allaah amrehemu), wakati akielezea khilafu iliyopo baina ya wanachuoni kuhusu uwajibu wa mke kumtumikia mume wake kama kupika, kufagia, kuosha nguo n.k.

[5]- Surat An-Nisaa/34.
[6]- Mishkaatul Maswaabih (3696).

Baada ya kutaja kauli ya wale wanaosema kwamba jambo hilo si kwa mwanamke na kuidhoofisha kauli hiyo akasema:

**(وَقِيلَ – وَهُوَ الصَّوَابُ – وُجُوبُ الْخِدْمَةِ؛ فَإِنَّ الزَّوْجَ سَيِّدُهَا فِي كِتَابِ اللَّهِ؛ وَهِيَ عَانِيَةٌ عِنْدَهُ بِسُنَّةِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَعَلَى الْعَانِي وَالْعَبْدِ الْخِدْمَةُ؛ وَلِأَنَّ ذَلِكَ هُوَ الْمَعْرُوفُ)**

**"Na imesemwa (nayo ndio kauli ya sawa) ni wajibu wake kumtumikia mume wake, kwa sababu mume (ametajwa) ndani ya Qur'an kuwa ni Bwana wake, na pia yeye ni mateka mbele ya mume wake kwa hadithi ya Mtume swala na salamu zimshukie, na (inafahamika kwamba) mateka na mtumwa ni wajibu juu kumtumikia (bwana wake), na kwa sababu kufanya hivyo ndio wema (ulio kusudiwa)[7]".**

Na Sheikh Albani Allaah amrehemu baada ya kunukuu maneno haya ndani ya kitabu chake **(Aadabu Zzafaa "Uk. 235")** akasema:

**(قُلْتُ: وَهَذَا هُوَ الْحَقُّ إِنْ شَاءَ اللهُ تَعَالَى أَنَّهُ يَجِبُ عَلَى الْمَرْأَةِ خِدْمَةُ الْبَيْتِ).**

**"Ninasema: hii ndio kauli ya sawa In Shaa Allaah Ta'alaa, kwamba ni wajibu juu ya mwanamke kuitumikia nyumba (ya mume wake)".**

Na akapinga kauli ya wanaosema kwamba mke ni kwa ajili ya kustarehe naye tu wala si wajibu wake kukutumikia.

**(وَقَوْلُ بَعْضِهِمْ: "إِنَّ عَقْدَ النِّكَاحِ إِنَّمَا اقْتَضَى الاسْتِمْتَاعَ لَا الاسْتِخْدَامَ" مَرْدُوْدٌ بِأَنَّ الاسْتِمْتَاعَ حَاصِلٌ لِلْمَرْأَةِ أَيْضًا بِزَوْجِهَا فَهُمَا مُتَسَاوِيَانِ فِيْ هَذِهِ النَّاحِيَةِ).**

[7]- Majmuu'l fataawa (Jz. 34, Uk. 90).

**“Na kauli ya baadhi yao: kwamba kufunga ndoa kunahukumilia kwenye kupata ladha tu kwa (mke) ni yenye kupingwa kwa sababu mwanamke pia hupata ladha kwa mume wake, kwa hiyo kwa upande huu wanalingana sawa[8]”.**

Lakini tukisema hivyo hatukusudii kumfanya mwanawake kama mfungwa wa gerezani n.k kama wanavyofanya baadhi ya wanaume ambao hawana matangamano mazuri wa wake zao.

Amesema sheikh Albani Allaah amrehemu:

(هَذَا وَلَيْسَ فِيْمَا سَبَقَ مِنْ وُجُوْبِ خِدْمَةِ الْمَرْأَةِ لِزَوْجِهَا مَا يُنَافِي اسْتِحْبَاب مُشَارَكَةِ الرَّجُلِ لَهَا فِيْ ذَلِكَ إِذَا وَجَدَ الفَرَاغَ وَالْوَقْتَ بَلْ هَذَا مِنْ حُسْنِ الْمُعَاشَرَةِ بَيْنَ الزَّوْجَيْنِ).

**“Zingatia haya, hakuna katika hayo yaliyo tangulia ambayo ni uwajibu wa mke kumtumikia mume kinachozuia kupendekezwa kwa mwanamme kutoa ushiriakiano (kumsaidia) yeye katika hilo pindi akipata muda na nafasi, na hilo ni miongoni mwa matangamano mazuri baina ya mume na mke[9]”.**

5. Kutunza siri za Mume: hasa yale yanayo fanywa kwa siri baina ya mume na mke, kwa sababu kuhadithia mambo hayo ni katika madhambi na kumhuzunisha mume wake, na kutunza siri ni miongoni mwa sifa za wanawake wema kama tulivyoona katika aya iliyo tangulia.

Imepokewa kutoka kwa Asmaa Bint yazid Allaah amridhie kwamba yeye alikuwa mbele ya Mtume swala na salamu zimshukie hali ya kuwa wanaume na wanawake wamekaa, Mtume swala na salamu zimshukie akasema:

---

[8]- Aadabu Zzafaaf (288).
[9]- Aadabu Zzafaaf (290).

«لَعَلَّ رَجُلًا يَقُولُ: مَا يَفْعَلُ بِأَهْلِهِ، وَلَعَلَّ امْرَأَةً تُخْبِرُ بِمَا فَعَلَتْ مَعَ زَوْجِهَا فَأَرَمَّ الْقَوْمُ " فَقُلْتُ: إِي وَاللهِ يَا رَسُولَ اللهِ، إِنَّهُنَّ لَيَقُلْنَ وَإِنَّهُمْ لَيَفْعَلُونَ قَالَ: " فَلَا تَفْعَلُوا فَإِنَّمَا مِثْلُ ذَلِكَ مِثْلُ الشَّيْطَانِ لَقِيَ شَيْطَانَةً فِي طَرِيقٍ فَغَشِيَهَا وَالنَّاسُ يَنْظُرُونَ»

**"Huenda mume akasimulia yale anayofanya na mke wake, na huenda mke akasimulia yale anayofanya na mume wake, watu wakanyamaza, nikasema (Asmaa): Ndio, Walaahi (naapa kwa Allah) ewe Mtume wa Allaah, wanawake wanasimulia na wanaume (pia) wanasimulia. Akasema: msifanye hivyo, hakika mfano wa hilo ni mfano wa shetani (wa kiume) amekutana na shetani (wa kike) njiani akamuingilia hali ya kuwa watu wanamuona[10]".**

Amesema As Sindi (Allaah amrehemu):

(قَوْلُهُ: "فَإِنَّما مِثْلُ ذَلِكَ" أَيْ: إِظْهَارُ مَا جَرَى بَيْنَ الْإِنْسَانِ وَأَهْلِهِ بِالْقَوْلِ، كَإِظْهَارِهِ بِالْفِعْلِ)

**"Kauli yake aliposema: (hakika mfano wa hilo) anakusudia: kudhihirisha mambo yaliyo pita (chumbani) baina ya mume na mke wake kwa kusimulia ni sawa na kuonyesha (jambo) hilo kwa vitendo)[11]".**

Hii ni ishara ya uovu wa jambo hilo na ukubwa wake mbele ya Allaah Ta'alaa mpaka limelingana sawa na mtu kufanya jimai na mke wake hadharani!

Nachukua fursa hii kuwanasihi wahubiri ambao hupenda kusimulia mambo ya chumbani huku wakiashiria kana kwamba wao hufanyiwa hivyo na wake zao na pia wana tabia hiyo pia, kwa madai ati wanasimulia neema za Mola wao! Wako wapi hawa na maneno hayo ya Mtume swala salamu zimshukie?!

---

[10]- Irwaaul ghaliil (2011).

[11]- Musnad Ahmad (Jz. 45, Uk. 565) hadithi (27584). Maneno ya chini ya ukurasa katika.

Haipasi kwa watu sampuli hii kutawanya mawaidha yao kwenye redio, runinga (television) n.k, achilia kupewa mimbari za misikiti kwa ajili ya kuongea na waislamu. **Ee Allaah tuongoze kwenye tabia njema.**

6. **Kudhihiri mbele ya mume wake kwa muenekano mzuri:** kiasi cha kufurahi mume wake pindi akimtazama, ndiyo Mtume swala na salamu zimshukie alipoulizwa ni yupi mmke wema?: Akasema:

«الَّتِي تَسُرُّهُ إِذَا نَظَرَ، وَتُطِيعُهُ إِذَا أَمَرَ، وَلَا تُخَالِفُهُ فِي نَفْسِهَا وَمَالِهَا بِمَا يَكْرَهُ»

**"Ambaye anamfurahisha mume wake akimtazama, anamtii akimuamrisha, na wala hapingani naye katika nafsi yake wala mali yake kwa jambo ambalo analichukia".**

Anakusudia kwamba anapomuita kitandani kwa ajili ya jimai mwanamke huyo hamkatalii kwa sababu hilo ni lenye kumchukiza mume wake na hiyo maana ya **"wala hapingani naye katika nafsi yake"**, na pia imetajwa maana nyingine kwamba hamsaliti mume wake kwa kufanya uzinifu na wanaume wa kando. Allaah atulinde. Na maana ya kwamba hafanyi kwenye mali yake jambo lenye kumchukiza mume ni kama vile kufanya matumizi au kutoa sadaka katika mali yake bila idhini ya mume wake.

7. **Asimruhusu mtu yeyote kuingia nyumbani kwake isipokuwa kwa idhini ya mume:** kama ilivyokuja katika hadithi:

«لاَ يَحِلُّ لِلْمَرْأَةِ أَنْ تَصُومَ وَزَوْجُهَا شَاهِدٌ إِلَّا بِإِذْنِهِ، وَلاَ تَأْذَنَ فِي بَيْتِهِ إِلَّا بِإِذْنِهِ، وَمَا أَنْفَقَتْ مِنْ نَفَقَةٍ عَنْ غَيْرِ أَمْرِهِ فَإِنَّهُ يُؤَدَّى إِلَيْهِ شَطْرُهُ»

**"Haifai kwa mwanamke kufunga (saumu) na hali ya kuwa mume wake yupo (katika mji) isipokuwa kwa idhini yake, wala asimruhusu yeyote kuingia nyumbani kwake isipokuwa kwa idhini yake, na mali yoyote aliyoitoa sadaka bila ya idhini (ya mume) wake atapewa yeye (mume) nusu yake[12]".**

Faida:

1) Haifai kwa mwanamke kumuingiza ndani ya nyumba yake mtu ambaye anafahamu kwamba mume wake haridhii mtu huyo kuingia humo, hata kama ni ndugu wa karibu, lakini wanawake wengi hili hawatekelezi matokeo yake anamruhusu mtu kuingia ndani pindi mume wake akitoka!.

2) Akiwa mwanamke ameruhusiwa na mume wake kutoa msaada katika chakula au pesa basi ni vizuri ajichunge katika utoaji wake, wala asipitilize kiwango cha kawaida (na kila watu wana kiwango chao) akamaliza pesa ya matumizi ya wajibu nyumbani, hakika kufanya hivyo ni makosa na akitoa kiasi kile cha kawaida atapata ujira yeye (kwa kutoa) na mumewe kwa sababu yeye ndiye mmiliki wa mali hiyo.

   Na ruhusa iko aina mbili: ruhusa ya jumla, kama kusema: "Akija mtu yeyote mwenye shida msaidie". Au ruhusu yenye udhibiti, mfano: "Usimsaidie mtu zaidi ya shilingi (2,000) au kilo 2 n.k", katika hali hiyo asitoe zaidi ya kiwango alichoambiwa isipokuwa kwa idhini ya mume wake.
   Ama akitoa mali ya mume wake bila idhini yake atapata madhambi. **Zingatieni hili.**

---

[12]- Bukhari (5195).

8. **Asimuombe mumewe wake Talaka bila sababu za msingi:** kwa sababu ya hadithi iliyo kuja kukataza jambo hilo:

«أَيُّمَا امْرَأَةٍ سَأَلَتْ زَوْجَهَا طَلَاقًا فِي غَيْرِ مَا بَأْسٍ، فَحَرَامٌ عَلَيْهَا رَائِحَةُ الْجَنَّةِ»

**"Mwanamke yeyote ambaye amemuomba mume wake talaka bila ya ubaya wowote (aliomtendea) ni haramu juu yake (kupata) harufu ya pepo[13]".**

Hii ndiyo adhabu ya mwanamke ambaye ameomba talaka ili kuachana na mume wake bila sababu za kisheria, siku ya kiama hapati harufu ya pepo. Pia afahamu mume kwamba yeye ni msimamizi na ataulizwa kuhusu mke na watoto wake, na mke ajuwe kwamba ameamrishwa kumtii mume wake na kuilea vizuri familia yake na kutoa juhudi katika kutengeneza nyumba yake.

Na kudai talaka huenda ikawa kwa kutamka maneno au kufanya vitendo ambavyo hatimaye mume huyo atashindwa kuishi naye, hili ni kwa sababu wengi katika hao hawajui haki zilizo juu yao katika kuwatekelezea waume zao, kwa hiyo wao wanaingia kwenye ndoa kwa makusudio mengine si yale yaliyo tajwa na Allaah Mola wao aliye waumba na mmoja wao akikosa kile alicho tarajia kukipata kwa mume huyo anadai talaka ili akajaribu bahati sehemu nyingine **kama wanavyodai!** Ee Mola wetu Mlezi Allaah, tupe katika wake zetu na wenetu yaburudishayo macho na utujaalie tuwe viongozi kwa watu wema.

9. **Kutodharau huduma zinzo tolewa na mume:** kwa sababu Mtume swala na salamu zimshukie ametaja wazi kwamba Allaah hamuangalii kwa jicho la huruma mwanamke ambaye

[13]- Sunan Abi Daud (2226).

hamsifu wala kumshukuru mume wake kwa huduma anazompatia.

Amesema:

«لا يَنْظُرُ اللهُ إِلَى امْرَأَةٍ لا تَشْكَرُ لِزَوْجِهَا وَهِيَ لا تَسْتَغْنِي عَنهُ»

**"Allaah hamuangalii (kwa huruma) mwanamke ambaye hamshukuru mume wake, na hali ya kuwa hajitoshelezi kumuacha yeye[14]".**

Huyu ni mwanamke muovu ambaye haifai kwa mwanamme kumuoa, na hawa ndiyo wale amabo utamtendea wema na hisani miaka mingi lakini akipata kutoka kwako kasoro au kero yoyote atasema: **(sijaona kutoka kwako wema wowote)** na wengine hufikia kusema: **(naona hapa napoteza muda tu!)**, haya yote ni kwa sababu hawajui makemeo haya wala hawako tayari kujifunza kwa sababu hawataki kupotez malengo yao!.

10. Asivue nguo zake katika isiyo kuwa nyumba ya mume wake: kwa kauli ya Mtume swala na salamu zimfikie:

« أَيُّمَا امْرَأَةٍ نَزَعَتْ ثِيَابَهَا فِي غَيْرِ بَيْتِهَا خَرَقَ اللَّهُ عَنْهَا سِتْرَهَا »

**"Mwanamke yeyote ambaye amevua nguo zake katika isiyo kuwa nyumba (makazi) yake Allaah atamuondolea yeye sitara (siku ya kiama)".**

Makusudio ya hapo ni mwanamke aliyevua nguo zake kwa ajili ya kufanya uzinifu au vitangulizi vya uzinifu na wanaume, lakini yule aliye punguza nguo zake mbele ya wanawake wenzie katika mazingira ya sitara haingii katika makemeo haya.

---

[14]- Angalia kitabu: [Silsila Ahaadithi Ssahiha (289)].

Na wakati alipoacha kumtii Allaah katika amri yake na kuacha kujisitiri mpaka akafikia kutoka ndani ya nyumba yake kwenda kwa mwanaume na akapata ujasiri wa kuvua nguo zake mbele yake kwa ajili ya kufanya zinaa (namuomba Allaah atuhifadhi) basi Allaah atamfedhehi mwanamke huyo siku ya kiama mbele ya viumbe wote.

Ni pia ni wajibu wake wajibu mwanamke:

1) kuwa na haya (aibu) mbele ya mume wake.
2) Asimkodelee macho (akamuangalia kama adui yake).
3) Kunyamaza pindi anapo zungumza.
4) Kujiepusha na mambo yenye kumuudhi.
5) Asimsaliti wakati anapokuwa mbali na nyumba yake.
6) Kudhihiri kwa mume wake akiwa ananukia harufu nzuri.
7) Kujizoesha kupiga mswaki mara kwa mara.
8) Kujipamba wakati anapokuwa na mume wake na kuacha kufanya hivyo akiwa mume hayupo.
9) Kuwajali jamaa wa mume wake na ndugu zake.
10) Kuthamini kidogo anachopewa na mume wake.

Allaah ndiye Mjuzi zaidi.

Ewe Allaah tupe wake wema watakao tusaidia katika
mambo ya Dini na Dunia yetu.

Alkhamisi 14/ramadhani/1441h – 7/5/2020m

Pongwe – Tanga

Tanzania.